

Kurudia Darasa la Tatu: Fomu ya Mapendekezo ya Kukata Rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1

Kwa mujibu wa sheria ya T.C.A. § 49-6-3115 na Kanuni ya 0520-01-03-.16 ya Bodi ya Elimu ya Jimbo (SBE), mzazi au mlezi wa kisheria wa mwanafunzi ambaye ametambuliwa kuwa anapaswa kurudia katika darasa la tatu kutokana na kupata alama ya kiwango "kinachokaribia kufikia matarajio" katika ukadiriaji kwenye sehemu ya ELA ya mjarabu wa TCAP ambao mwanafunzi amefanya hivi karibuni, anaweza kukata rufaa moja kwa moja kwenye Idara.

Masharti ya kukata rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1 ni pamoja na:

- Mzazi au mlezi wa kisheria wa mwanafunzi anakubali kuwa alipewa noti ya masharti yote ya kukata rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1 na anakubali kuwa mwanafunzi wake atazingatia masharti yote ya kukata rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1 ikiwa uamuzi wa kurudia darasa utabatilishwa.
- Mwanafunzi amepata alama sawa au zaidi ya asilimia arobaini (40%) kwenye mjarabu uliotolewa majira ya kuchipua wa TN-URS (Aimsweb) unaosimamiwa na LEA au shule ya umma inayojitegemea.
- Mkuu wa shule ya mwanafunzi anakubali kuandaa mpango wa kimasomo wa ufidiaji, kwa kushirikiana na walimu wa mwanafunzi na timu ya IEP au timu ya 504 ikiwa inahusikaa, kwa mwanafunzi huyo. Mpango wa kimasomo wa ufidiaji utajumuisha mikakati inayotegemea ushahidi na maoni kutoka kwa wazazi wa mwanafunzi na wafanyakazi wengine wa shule wanaohusika.
- Mwalimu wa sasa wa ELA na mkuu wa shule wa mwanafunzi wanatoa pendekezo kwa kauli moja kuwa mwanafunzi aruhusiwe kujiunga na darasa la 4.
- LEA ya mwanafunzi au shule ya umma inayojitegemea inakubali kutoa huduma za mafunzo ya kiwango cha juu, ya uwiano wa chini kwa mwanafunzi kwa kipindi cha mwaka mzima wa darasa la nne (4) kwa mwanafunzi.

Ili kuwasilisha rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1, mzazi au mlezi wa kisheria au afisa wa shule ambaye amepokea idhini iliyoandikwa kwa niaba ya mzazi au mlezi wa kisheria, anaweza kuwasilisha fomu ya kukata rufaa katika ukurasa wa Idara wa [Uboreshaji wa Mafunzo](#).

Wakati wa kuwasilisha rufaa, mwasilishaji atahitaji kupakia ukurasa ufuatao wa sahihi ambao umekwisha kujazwa na mkuu wa shule wa mwanafunzi na mwalimu wa ELA ili kuonyesha kukubaliana na masharti yaliyotajwa ya kukata rufaa.

Fomu ya Sahihi ya Kukata Rufaa kwa Misingi ya Sababu ya 1

Jina la Kisheria la Mwanafunzi

Jina la Wilaya ya Shule

Kitambulisho cha Mwanafunzi (Nambari ya tarakimu 7)

Jina la Shule

Mkataba Mkuu wa Kutengeneza Mpango wa Kielimu wa Ufidiaji, Kutoa Mafunzo na Mapendekezo ya Kuruhusiwa Kujiunga na Darasa la Nne.

[Kanuni ya Bodi ya Elimu ya Jimbo \(SBE\)](#) inamtaka mkuu wa shule ya mwanafunzi kukubali kuandaa mpango wa kimasomo wa ufidiaji kwa mwanafunzi aliye katika hatari ya kurudia darasa. Mpango wa kimasomo wa ufidiaji utauandwa kwa ushirikiano na walimu wa mwanafunzi, na tima IEP au timu ya 504 ikiwa inahusika na unaweza pia kujumuisha maoni kutoka kwa wazazi wa mwanafunzi, mshauri wa shule au wafanyakazi wengine wa shule wanaohusika. Mpango wa kimasomo wa ufidiaji utajumuisha mikakati inayotegemea ushahidi iliyoundwa kulingana na mahitaji ya kujifunza ya mwanafunzi. Mikakati hii ya inayotegemea ushahidi itajumuisha angalau mojawapo ya mambo yafuatayo:

- I. Maboresho ya mikakati ya sasa ya mafunzo au nyenzo za kufundishia za ubora wa hali juu;
- II. Muda wa ziada wa mafunzo;
- III. Marekebisho ya kazi ya darasani ya mwanafunzi ili kuhakikisha kuwa mwanafunzi anapokea maelekezo kutoka kwa mwalimu mwenye kiwango cha ufaulu wa jumla wa matarajio yaliyo juu (kiwango cha 4) au zaidi ya matarajio (kiwango cha 5); au
- IV. Uwekaji wa mwanafunzi huyo katika darasa lenye ukubwa uliopunguzwa.

Sheria ya SBE pia inahitaji LEA au shule ya umma inayojitegemea kukubali kutoa mafunzo ya kiwango cha juu, ya uwiano wa chini kwa mwanafunzi huyo kwa kipindi chote cha darasa la nne.

Sheria ya SBE pia inahitaji mkuu wa shule wa sasa wa mwanafunzi kutoa pendekezo ya kuwa mwanafunzi aruhusiwe kujiunga na darasa la 4.

Sahihi yako iliyo hapa chini inaonyesha pendekezo lako kwa mwanafunzi aruhusiwe kujiunga na darasa la 4 na kukubali kwako kwa masharti yaliyo hapo juu.

Jina la Mkuu wa Shule

Sahihi ya Mkuu wa Shule

Tarehe

Pendekezo la Mwalimu wa ELA la Kuruhusiwa Kujiunga na Darasa la Nne

Sheria ya SBE inahitaji mwalimu wa sasa wa ELA wa mwanafunzi huyo kutoa pendekezo la kuwa mwanafunzi huyo aruhusiwe kujiunga na darasa la 4.

Sahihi yako iliyo hapa chini inaonyesha pendekezo lako kwa mwanafunzi huyo aruhusiwe kujiunga na darasa la 4.

Jina la Mwalimu wa ELA

Sahihi ya Mwalimu wa ELA

Tarehe